USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

Washiriki waliohudhuria mkutano wa kupanga shughuli za mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira (MUM) kwa mwaka wa kwanza. Mkutano ulifanyika Novemba 3 -5, 2021 Mkoani Iringa. Mpiga picha: Yussuf Kajenje, USAID/MUM

TANZANIA

MRADI WA USAID/MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA (MUM)

Ukifanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na taasisi za umma, sekta binafsi pamoja na wananchi, Mradi wa USAID/ Maji na Usafi wa Mazingira (MUM) unaofadhiriwa na Serikali ya Watu wa Marakeni, utafanya kazi na wadau mbalimbali katika ngazi ya taifa, mkoa na wilaya kuboresha mifumo inayotumika katika kupanga, kugharamia na kutekeleza shughuli mbalimbali zinazolenga kuboresha usimamizi wa rasilimali za maji na kupanua na kurahisisha upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mwili pamoja na mazingira. Katika utekelezaji huu, MUM itatumia mikakati minne inayotegemeana, ambayo ni pamoja na: kuimarisha umilikaji wa jamii wa huduma kwa kuwashirikisha wadau mara kwa mara kadri iwezekanavyo, kuimarisha mifumo ya taasisi husika na huduma zitolewazo, kwa kutumia misingi/ kanuni za soko, kujifunza kutokanan na vitendo kadri utekelezaji unavyoendelea katika wilaya 10 za mikoa minne ambayo ni Morogoro, Iringa, Njombe na Rukwa; katika mabonde ya Mto Rufiji, Ziwa Nyasa na Ziwa Rukwa. Mradi unalenga kufanya yafuatayo katika wilaya zilizoainishwa/zinazolengwa:

- **Lengo la Kwanza (SO1):** Kuongeza upatikanaji wa huduma endelevu za maji zinazoendeshwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Mijini (UWSSAs)
- **Lengo la Pili (SO2):** Kuongeza upatikanaji wa fedha za kugharamia huduma za maji, usafi wa mwili na mazingira
- **Lengo la Tatu (SO3):** Kuimarisha masoko ya bidhaa na huduma zinazohitajika kwa ajili ya kuboresha usafi wa mazingira na mwili.
- **Lengo la Nne (SO4):** Kuimarisha Bodi za Mabonde ya Maji (BWBs) Pamoja na Jumuiya za Watumia Maji (WUAs) ili kuziwezesha kusimamia ipasavyo rasilimali za maji,

BAJETI
Dola Milioni 25 (Zikiwemo Dola Milioni 3 za ruzuku)

MUDA WA UTEKELEZAJI
Agosti 2021 – Agosti 2026

ENEO LA UTEKELEZAJI
USAID/Tanzania MUM inafanya kazi katika wilaya 10 za mikoa ya Morogoro, Iringa, Njombe na Rukwa, katika Mabonde ya Maji ya Wami-Ruvu, Rufiji, Ziwa Rukwa na Ziwa Nyasa.

WADAU KATIKA UTEKELEZAJI
Tetra Tech ARD, FSG, WISE Futures na IRIS Group kwa kushirikiana na RUWASA, LGAs, CBWSOs, BWBs, WUAs na Sekta binafsi

ANUANI (OFISI ZA USAID)
Mhandisi Francis Mtitu
COR, USAID/Tanzania
P.O. Box 9130, Dar es Salaam, Tanzania
+255 (0) 713 494 916
fmtitu@usaid.gov

ANUANI (OFISI ZA MUM)
Mhandisi Bigambo Nandiga
Mkuu wa Mradi wa MUM
P.O. Box 2590, Iringa, Tanzania
+255 (0) 782 949 677
Bigambo.Nandiga@tetratech.com

KWA TAARIFA ZAIDI
Website: www.usaid.gov/tanzania
Facebook: USAIDTanzania
Twitter: @USAIDTanzania

- **Lengo Mtambuka:** - Kuendeleza usawa wa kijinsia na kuwashirikisha vijana na wanawake katika usimamizi wa rasilimali za maji kwa matumizi mbalimbali na upatikanaji wa huduma husika.

MATOKEO YANAYOTARAJIWA

Lengo la Kwanza (SO1): Kuongeza upatikanaji wa huduma za maji na usafi

- RUWASA iongeze uwezo wake wa kitaasisi katika kupanga, kufuatilia na kusimamia huduma za maji vijijini
- Kupunguza muda wa kutopatikana kwa huduma ya maji katika willaya husika kutokana na hitilafu zinazoweza kujitokeza kwenye miradi ya maji
- Kuwezesha kuwepo kwa muundo mpya wa matengenezo na uendeshaji wa miradi ya maji vijijini kwa wilaya zote husika katika eneo la mradi
- Uboreshaji wa maduhuli kwa watoa huduma za maji katika maeneo ya mradi
- Kuongezeka uwezo wa kiutendaji wa mamlaka za maji mijini (sawa na kuziwezesha kupanda kutoka daraja moja hadi lifuatalo- kwa mfano kutoka Daraja C kwenda B au B kwenda A)
- Kuboresha ufuatiliaji wa huduma za maji kwenye ngazi ya wilaya, mkoa na taifa
- Kuimarika na kuwepo majadiliano ya mara kwa mara kati ya serikali na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, yakizingatia vielelezo vitokanavyo na uchambuzi na takwimu bora za maji na usafi wa mazingira.

Lengo la Pili (SO2): Kuongeza upatikanaji wa fedha za kugharamia huduma za maji, usafi na mazingira

- Angalao Mamlaka 10 za maji na usafi wa mazingira mijini pamoja na Wakala wa Maji vijini (RUWASA) angalao katika wilaya tano ziweze kuandaa maandiko yanayokidhi vigezo vya kupata fedha kutoka Mpango wa Ushirikianao wa Kifedha na Serikali ya Marekani na/au asasi nyingine za fedha.
- Vikundi vya wajasiriamali wadogo na wa Kati angalao 15 vinapata fedha kutoka asasi zinazotoa pesa, zikiwemo benki na vyanzo vingine. Angalau vikundi 8 kati ya hivyo viwe vikiongozwa na wanawake au vijana.
- Kuwepo na ongezeko la asilimia 30 ya rasilimali fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mabonde ya Maji kuyawezesha kutekeleza shughuli za usimamizi wa rasilimali za maji.

Lengo la Tatu (SO3): Kuimarisha masoko ya bidhaa na huduma zinazohitajika kwa ajili ya usafi

- Kuwepo ongezeko la asilimia 25 la idadi ya watu katika wilaya zilizoko chini ya mradi ambao wanatumia vyoo au miundombinu bora ya usafi wa mazingira katika kaya zao
- Kuwepo na huduma na bidhaa nzuri za usafi wa mazingira na mwili zilizo bora katika wilaya zote za mradi
- Angalao wajasiriamali 25 wanaotoa huduma na bidhaa za usafi wanaongeza mapato na tija katika biashara zao.
- Kuwepo ushiriki mpana wa wanawake na vijana kama wataalamu katika soko la bidhaa na huduma za usafi wa mazingira

Lengo la Nne (SO4): Kuimarisha Bodi za Mabonde ya Maji (BWBs) Pamoja na Jumuiya za watumia Maji (WUAs) ili kuziwezesha kusimamia rasilimali za maji

- Kuboresha uwezo wa Bodi za Mabonde ya Maji (BWBs) katika kusimamia rasilimali maji, hususan katika zama hizi za mabadiliko ya tabia nchi
- Bodi za Mabonde ya Maji na Jumuiya za Watumia Maji ziweze kuongeza mapato yao kutokana na maduhuli yapatikanayo kupitia malipo kutoka kwa watumia maji
- Bodi za Mabonde ya Maji na Jumuiya za Watumia Maji ziweze kuwa na ongezeko la bajeti inayohitajika katika uendeshaji na utekelezaji wa mipango yao ya usimamizi wa rasilimali maji
- Kuwepo ongezeko la asilimia 30 ya idaidi ya watu wanaonufaika kutokana na utekelezaji wa hatua za usimamizi wa rasilimali ya maji, katika zama za mabadiliko ya tabia nchi
- Kuwapo upatikanaji wa uhakika wa huduma za maji katika miji midogo katika eneo la mradi